JANUARI 2022



AJIRA ZA KIGENI

MWONGOZO WA TAARIFA KUHUSU USALAMA WA WAFANYIKAZI WAHAMIAJI

GLOBAL FUND TO END MODERN SLAVERY

IOM UN MIGRATION

MUHTASARI

Wafanyikazi wahamiaji kutoka Kenya wanachangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Uhamiaji unaosimamiwa ipasavyo hunufaisha nchi za asili, za usafiri na za kigeni kupitia ustawishaji wa ujuzi na kuongezeka kwa mapato ya familia ya wale wanaofanya kazi pamoja na ongezeko la pato la taifa (GDP) kupitia pesa zinazo tumwa chini.

Licha ya manufaa hayo, wanaotafuta kazi na Wafanyikazi wahamiaji wanaendelea kukabiliwa na mazingira duni ya kazi pamoja na kubaguliwa, baadhi yao hukosa mahitaji ya kimsingi na ya kiuchumi, haki za kijamii na kitamaduni, wakati mwingine wanakabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia na katika hali mbaya zaidi huripotiwa vifo vya ajabu na visivyo eleweka.

Serikali kwa ushirikiano na washikadau mashuhuri kama vile Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), imeanzisha michakato na kupiga hatua kadhaa za kuhakikisha ustawi na usalama wa wafanyikazi kutoka Kenya wanaotafuta riziki katika nchi za kigeni haswa maitaifa ya ughaibuni. Hata hivyo, wafanyikazi wahamiaji wanaendelea kukabiliwa na changamoto hizi kutokana na mazoea yasiyo ya kimaadili ya kuajiri pamoja na kutokuwa na taarifa mahususi kuhusu uhamiaji salama wa Wafanyikazi katika nchi za kigeni.

Mwongozo huu wa habari hivyo basi, unaziba pengo la kutokuwepo kwa taarifa kuhusiana na ajira za kigeni kwa kutoa taarifa sahihi kuhusu njia za kisheria za uhamiaji na ufahamu unaohitajika sana juu ya mazoea yasiyo ya kimaadili ya kuajiri wafanyikazi. Hasa mwongozo huu wa taarifa unashirikisha taarifa muhimu ambazo wanaotafuta kazi na Wafanyikazi wanaotarajiwa kuhamia nchi za kigeni wanahitaji kujua kuhusu kabla ya kuondoka, awamu ya kusafiri, na awamu ya kufanya kazi na kuishi katika mataifa haya ya kigeni, kurejea na kuunganishwa tena na jamii baada ya kuhitimisha wajibu wa kazi na pia mwongozo utangazia baadhi ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara katika uhamiaji wa Wafanyikazi.

YALIYOMO

MUHTASARI ..... **Error! Bookmark not defined.**

YALIYOMO II

ORODHA YA VIELEKEZO III

ORODHA YA MAJEDWALI III

UHAMIAJI WA KAZI 4

UTANGULIZI 4

HATUA SALAMA ZA UHAMIAJI WA WAFANYIKAZI 5

AWAMU YA KABLA YA KUONDOKA NCHINI 7

MCHAKATO WA KUTAFUTA NA KUPATA KAZI 7

WANAOTAFUTA KAZI WANATAKIWA KUZINGATIA NINI 9

JE, UTAJUAJE WAKALA HALISI WA AJIRA? 10

HATUA MUHIMU KABLA YA KUONDOKA NCHINI 11

MKATABA WA AJIRA 13

MTAALA WA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NYUMBANI 14

MAFUNZO KABLA YA KUONDOKA NCHINI 14

AWAMU YA USAFIRI 16

ORODHA YA MAMBO MUHIMU KABLA YA KUONDOKA NCHINI 16

TARATIBU ZA UWANJA WA NDEGE 17

BAADA YA KUPATA KIBALI CHA KUONDOKA KWENYE UWANJA WA NDEGE 19

KUFANYA KAZI NA KUISHI NJE YA NCHI 21

NINI WAFANYIKAZI WANAPASWA KUZINGATIA 21

KUTUMA PESA KATIKA NCHI ASILI 23

KANUNI ZA KAZI 24

FOMU YA NEA YA KUTOA TAARIFA ZA TAHADHARI 24

JINSI YA KUPATA HABARI 24

KUREJEA NA KUUNGANIKA TENA NA JAMII 26

ORODHA YA VITU VINAVYOHITAJIKA KABLA YA KUREJEA 26

MAANDALIZI KABLA YA KURUDI NYUMBANI 27

SAFARI YA KUREJEA NCHI ASILIA 27

KUUNGANA NA JAMII BAADA YA KUREJEA 28

JINSI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO 29
MASWALI YA MARA KWA MARA KUHUSU UHAMIAJI WA WAFANYIKAZI 30
HITIMISHO 35

ORODHA YA VIELEKEZO

Kielelezo cha 1: Hatua za Uhamiaji wa Wafanyikazi _____ 6

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali la 1: Vyeti vinavyohitajika Mahitaji kabla ya usafiri na mahali pa kupata _____ 33

UHAMIAJI WA KAZI

UTANGULIZI

Kazi katika nchi za kigeni ni chanzo cha ajira na riziki kwa wafanyikazi wahamiaji, na mojawapo ya njia kuu za kuimarisha teknolojia na uhamisho wa ujuzi kati ya nchi. Faida za uhamiaji wa vibarua hufurahiwa na wafanyikazi wahamiaji, familia, jamii zao; serikali za majimbo na kitaifa; mashirika yasio ya kiserikali; na mashirika ya kikanda. Kenya kama nchi nyingi zinazokuakiuchumi inaendelea kushuhudia uhamiaji wa wafanyikazi katika nchi zingine. Sababu zinazopelekea mtindo huu ni pamoja na: viwango vya juu vya ukosefu wa ajira pamoja na hali duni ya kijamii, kiuchumi na kimazingira nchini. Mambo yanayovutia ni pamoja na fursa za kuishi maisha bora, mishahara ya juu, ubora wa elimu na huduma za afya katika nchi za uhamiaji.

Maeneo na nchi zinazovutia Wafanyikazi kutoka Kenya ni pamoja na Mashariki ya Kati, Marekani, Kanada, Australia na Ulaya. Wafanyikazi hawa hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi hasa kupitia uhamishaji wa maarifa, ujuzi na maendeleo ya kiteknolojia. Kwa hivyo Kenya inapata faida kubwa kutokana na uhamiaji wa wafanyikazi katika nchi za kigeni.

Licha ya manufaa makubwa yanayoletwa nchini kutokana na uhamiaji wa vibarua, wafanyikazi wa Kenya katika mataifa haya ya kigeni wanaendelea kukabiliwa na changamoto nyingi katika nchi za uhamiaji. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na: ukiukwaji wa haki za kimsingi za Wafanyikazi wahamiaj, ukosefu wa data sahihi za kisasa na za kuaminika na taarifa juu ya uhamiaji wa kazi na Wafanyikazi wahamiaji, ukosefu wa njia madhubuti za kuwarejesha na kuwaunganisha tena wafanyikazi wahamiaji.

Kenya imeendelea kuangazia mipango inayolenga hasa kushughulikia masaibu ya wafanyikazi walio katika hali ya dhiki na wale wanaotendewa mabaya na ukiukwaji wa haki zao za kimsingi. Mojawapo ya suluhu ni utoaji wa taarifa ya kisasa na ya kuaminika juu ya uhamiaji wa wafanyikazi.


HATUA SALAMA ZA UHAMIAJI WA WAFANYIKAZI

Kuna hatua muhimu ambazo sharti zizingatiwe kabla ya kuondoka katika nchi asili, awamu ya usafiri, awamu ya kufanya kazi katika nchi za kigeni na vile vile wakati wa kurejea na kujiunga tena na jamii katika nchi asili.

Uhamiaji uliosalama unamaanisha kuwa wanaotarajia kufanya kazi nje ya nchi wanalindwa dhidi ya hatari zozote zinazohusiana na afya zao, hali ya kisheria au maisha katika hatua zote za mchakato wa uhamiaji. Pia inamaanisha kuwa wahamiaji wanapata huduma za kijamii na afya.

Kielelezo cha 1 kwenye ukrasa ufuatao kinatoa muhtasari wa hatua salama za uhamiaji wa leba

Kielelezo cha 1: Hatua za Uhamiaji wa Wafanyikazi



AWAMU YA KABLA YA KUONDOKA NCHINI

Hii ni hatua muhimu ambayo kwa kiasi kikubwa huamua usalama na ustawi wa baadaye wa mfanyikazi katika nchi za kigeni. Awamu ya kabla ya kuondoka inahusu muda ambao anayetafuta kazi anawasilisha ombi la kazi iliyo wazi katika nchi ya kigeni, kisha baada ya maombi ya kazi kuzingatiwa hatua ya kupitia mchakato wa kuajiri, kupata kazi hadi atakapokuwa tayari kuondoka nchini na kuanza kazi mpya katika soko la ajira la kigeni.

MCHAKATO WA KUTAFUTA NA KUPATA KAZI

1. Tafuta tangazo la kazi ilio wazi

Nafasi za kazi hutangazwa kupitia

i. Wakala wa Uajiri wa Kibinafsi (PRAs)
ii. Tovuti mbalimbali kama www.neims.go.ke
iii. Kupitia vyombo vya habari
iv. Juhudi za mtu binafsi au/na rufaa

TANBIHI Unaweza kupata taarifa za mawasiliano za Wakala wa Uajiri wa Kibinafsi (PRAs) ambao wamesajiliwa na kuidhinishwa na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA) kwenya tovuti hii; https://neaims.go.ke/EmploymentAgencyList.aspx

2. Kulinganisha Kazi na Ujuzi

Wanaomba kazi wanatakiwa kujisajili kwenye tovuti ya Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEAIMS) kupitia www.neaims.go.ke. Waombaji kazi waliosajiliwa kwenya tovuti hii wanapaswa kufuatia mara kawa mara ili kutambua kazi zilizotumwa na Waajiri na mashirika ya kuajiri kwa ajili ya kutuma maombi. Wasifu huhakikiwa ili kuendana na mahitaji ya kazi na ujuzi uliowasilishwa na waombaji kazi waliohitimu na wao huorodheshwa tayari kwa kupigwa msasa.

3. Waajiri kuchambua maombi ya kazi

Mashirika ya uajiri huchambua maombi ya kazi na kusambaza wasifu za kazi(CV) zilizoorodheshwa kwa mwajiri mtarajiwa kwa hatua nyingine. Waajiri kisha huchagua wale walio waliohitimu na kuwasiliana na mashirika ya kuajiri yaliyoidhinishwa.

4. Walioorodheshwa wanaharifiwa kwa mahojiano

Waombaji kazi walioorodheshwa wanawasiliana na wakala wa kuajiri walioidhinishwa kupitia barua pepe, simu n.k.

TANBIHI Jihadhari na arifa ghushi na uthibitishe kila wakati kama Wakala ameidhinishwa na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA) tembelea tuvuti www.nea.go.ke kwa taarifa zaidi kuhusu Wakala.

5. Mafunzo ya Kabla ya mahojiano

Katika baadhi ya matukio waombaji kazi walioorodheshwa hualikwa kwa mafunzo ya kabla ya mahojiano ili kuboresha ujuzi wao wa mahojiano. Shirika la Maendeleo ya Vijana (Youth Enterprise Fund) na baadhi ya mashirika ya Ajira kwa kawaida huchukua jukumu hili

6. Kufanya Mahojiano

Mwajiri mtarajiwa huwasilisha tarehe ya mahojiano, mahali na wakati kwa wakala wa uajiri ambao huwafahamisha watahiniwa. Mahojiano hufanywa na mwajiri mtarajiwa au kupitia wakala wao ikishuhudiwa na mashirika ya kuajiri.

7. Watahiniwa huchaguliwa

Watahiniwa waliofaulu huarifiwa kupitia njia zinazofaa. Kisha wanaanza shughuli za kabla ya kuondoka, vipimo vya matibabu na uthibitisho. Mtahiniwa pia anapaswa kuthibitishwa na Wizara ya Leba chini.

8. Mafunzo ya Kabla ya Kuondoka nchini

Watahiniwa waliofaulu wanaarifiwa kuhusu mahali, wakati na tarehe ya mafunzo ya kabla ya kuondoka na mashirika ya kuajiri.

WANAOTAFUTA KAZI WANATAKIWA KUZINGATIA NINI

1. Mawakala wa Kuajiri ambao hawajasajiliwa

Usitumie mashirika ya kuajiri ambayo hayana leseni na hayajaidhinishwa na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA). Orodha ya mashirika yaliyoidhinishwa yanaweza kupatikana kwenye tuvuti ya shirila hilo: www.neaims.go.ke

2. Kutoza Ada Kupita Kiasi kilichoruhusiwa na sheria

Mwajiri anaweza lipa gharama zinazohusiana na usafiri, uchunguzi wa matibabu, vyeti vya afya, nyaraka rasmi n.k. Hata hivyo, katika baadhi ya matukio, unaweza kuhitajika kuchangia baadhi ya gharama. Ikiwa una shaka, thibitisha na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA) kupitia barua pepe info@nea.go.ke au tembelea ofisi za uajiri za NEA

3. Vibali vya Kazi na Mikataba

Kamwe usichukue ofa ya kazi ikiwa mwajiri hajakupokeza mkataba wa ajira uliotiwa Sahihi au ikiwa anasema kuwa mkataba wa ajira hauhitajiki. Bila mkataba, wewe utakua ni mfanyikazi ambaye hana hati na haki zako katika nchi unakoenda zitapunguzwa au kutumiwa vibaya.

4. Elewa masharti yote ya mkataba wa ajira

Hakikisha unaelewa masharti yote ya mkataba wa ajira kabla ya kuutia sahihi. Unapaswa kujua kama mwajiri atakuwa akikupa chakula cha bure, malazi n.k.

5. Visa halali ya Kazi

Hakikisha unapata visa halali ya kazi kabla ya kuondoka nchini. Kumbuka, hairuhusiwi kufanya kazi katika nchi ya kigeni kwa kutumia aina zingine za visa kama vile visa ya watalii au visa ya kutembelea nchi kwa kifupi.

6. Nakala za Nyaraka Muhimu.

Ili kufanya kazi katika nchi za kigeni kuna mahitaji tofauti kulingana na aina ya kazi. Walakini, yafuatayo ni mahitaji ya kimsingi kwa kazi zote: -

i. Pasipoti ambayo ni halali kwa angalau miaka miwili
ii. Mkataba wa kazi
iii. Kibali cha kazi
iv. Vyeti vya matibabu
v. Vyeti vya taaluma na elimu

JE, UTAJUAJE WAKALA HALISI WA AJIRA?

Kabla ya kuwasiliana na Wakala wowote wa Uajiri wa Kibinafsi, Hakikisha iwapo wakala huyo ameidhinishwa au amepewa leseni na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA) na ana agizo linalofaa la kazi na mtu nayewasiliana nawe ameunganishwa kihalali na wakala aliyeidhinishwa. Ikiwa una shaka, thibitisha kila wakati kwenye orodha ya Mawakala Walioidhinishwa kwenye tovuti www.neaims.go.ke

.Ikiwa wakala hajaorodheshwa kwenye orodha ya NEA inamaanisha kuwa ni Wakala Ambaye hajaidhinishwa

Thibitisha kama wakala,

i. Ana ofisi
ii. Imesajiliwa kama Kampuni ya Dhima ndogo na msajili wa Makampuni
iii. Imepewa leseni na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA)
iv. Hutoza ada au komisheni yoyote

Jihadharini na Utapeli wa Kazi

Walaghai wanaolenga wanaotafuta kazi wamebuni njia za kiteknolojia za kupora pesa kwa kisingizio cha kutoa kazi zinazolipa vizuri. Kadiri muda unavyopita, wamebadilisha mbinu hadi wanaweza kujifanya kuwa halali na kuwalaghai Wakenya wasio na fahamu kutuma pesa, mara nyingi kupitia huduma za pesa za rununu kama vile MPESA kwa matumaini ya kuhitimu hadi hatua inayofuata ya mahojiano.

Mchakato unahusisha baadhi ya mbinu za kisasa ili kuonekana kuwa asili na halali. Kwanza, watasajili jina la kikoa (domain) maalum kama vile "nfano.co.ke" kwa kawaida sawa na jina la kampuni bandia litakalotumiwa. Hii inahakikisha kwamba wanatumia barua pepe ambayo inaonekana rasmi kama vile "info@mfano.co.ke".

Kwa hivyo wanaotafuta kazi wanahitaji kuwa makini na kila wakati kuthibitisha ushauri wa kazi. **USITUMIE** pesa kuwezesha mchakato wowote wa kutafuta ajira.

HATUA MUHIMU KABLA YA KUONDOKA NCHINI

Kabla ya kuondoka nchini, ni sharti kujifunza mambo muhimu kama vile:- vinavyokubalika kubebwa ukisafiri, kanuni za usafiri, mafunzo ya kabla ya kuondoka nchini, kanuni za uwanja wa ndege na taratibu za ndege n.k. Katika sehemu hii tunatoa taarifa muhimu kuhusu mambo unayohitaji kufanya kabla ya kuondoka kwenda kufanya Kazi ya kigeni.

1. Baada ya kuhitimu mahojiano

Uchunguzi kamili wa matibabu unafanywa kulingana na mahitaji ya waajiri. Wakala wa uajiri wa Kenya hutuma ripoti hii ya matibabu kwa wakala katika nchi ya kigeni ambaye huthibitisha.

2. Barua ya ofa inatumwa

Ikiwa wakala wa uajiri katika nchi ya kigeni ameridhika na ripoti ya matibabu basi atatoa barua ya ofa. Barua hii hutumwa kwa wakala wa uajiri wa Kenya ambaye hushirikiana na mfanyikazi mtarajiwa.

3. Kukubalika kwa ofa

Mtahiniwa anapaswa kusoma na kuelewa barua ya ofa kabla ya kutia sahihi. Mtu anapaswa kutafuta usaidizi na ufafanuzi kutoka kwa wakala au hata Wizara ya Leba iwapo watahitaji ushauri kabla ya kutia sahihi kukubali.

4. Kutumwa kwa mkataba

Barua ya ofa iliyokubaliwa kisha hutumwa kwa wakala katika nchi ya kigeni ambaye hutayarisha mkataba wa kazi. Kisha mkataba hutumwa kwa wakala wa Kenya ili kumpokeza mfanyikazi matarajiwa.

5. Kutia sahihi mkataba

Mfanyikazi anapaswa kusoma na kuelewa mkataba kabla ya kutia sahihi. Mtu anapaswa kutafuta ushauri na ufafanuzi kutoka kwa wakala, NEA au hata Wizara ya Leba iwapo atahitaji maelekezo kabla ya kutia sahihi ili kukubali. Usitie sahihi mkataba ulioandikwa kwa lugha usiyoielewa.

6. Uthibitisho

Baada ya hayo mfanyikazi mtarajiwa anapaswa kuhidhinishwa na Wizara ya Leba nchini Kenya. Ili kuhidhinishwa, inahitaji mkataba uliotiwa sahihi, dhamana ya usalama na ripoti ya matibabu. Uthibitisho unafanywa kibinafsi katika ofisi ya Leba.

7. Tiketi ya ndege na VISA zinatumwa

Wakala katika nchi ya kigeni hutuma Tiketi ya Ndege kwa wakala wa uajiri wa Kenya kisha hupokezwa kwa aneenda kufanya kazi ugenini.

8. Mafunzo kabla ya kuondoka nchini

Mkenya aliyepata kazi ugenini anapaswa kuhudhuria mafunzo ya kabla ya kuondoka chini. Kuna taasisi mbalimbali za mafunzo zilizoidhinishwa na Mamlaka ya Taifa ya Mafunzo ya Viwanda (NITA). Kwa taarifa zaidi kuhusu ordha ya taasisi hizi, tembelea tuvuti ya NITA kwenya www.nita.go.ke

MKATABA WA AJIRA

Unachohitaji kujua kuhusu Mkataba wa Ajira

i. Lazima utie sahihi kwa Makubaliano ya Kazi au Mkataba na Wakala wako wa Kuajiri na Mwajiri kabla ya kuondoka nchini. Mkataba uliotiwa sahihi utahakikisha ulinzi wa haki zako wakati wa kazi ugenini.

ii. Hakikisha unaelewa masharti yote yaliyofafanuliwa katika Mkataba. Uliza mtu unayemwamini akueleze waziwazi unapohitaji usaidizi ili kuhakikisha usalama na ustawi wako.

Sahihi na ridhaa zifuatazo zinapaswa kuwa kwenye makubaliano.

i. Sahihi ya mwajiri
ii. Sahihi ya wakala katika nchi ya kigeni
iii. Sahihi ya wakala nchini Kenya
iv. Sahihi ya mfanyikazi
v. Sahihi ya shahidi

TANBIHI:

Haupaswi kupata visa ya kibinafsi / ya utalii / likizo kutoka kwa marafiki au jamaa kama njia ya kutoka nchini kwa ajili ya kuajiriwa. Hakuna sheria zinazotetea masuala ya ustawi wa wasafiri kama hao wanaopatikana wakifanya kazi katika nchi za kigeni. Kwa hivyo, sio salama na haifai.

MTAALA WA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NYUMBANI

Mtaala wa Usimamizi wa Huduma ya Majumbani unashughulikia changamoto zinazowakabili watu wanaofanya kazi katika kaya na taasisi za kibinafsi kama vile nyumba za watoto, hospitali na taasisi za mabweni. Inalenga kuandaa Wafanyikazi waliohitimu, wenye tajriba, na wenye afya bora na ujuzi katika kazi za nyumbani. Wakenya wote wanaotaka kufanya kazi katika nchi za kigeni lazima wapitie kozi hiyo. Taasisi mbalimbali zimepewa ithibati ya kutoa mafunzo hayo. Orodha ya vituo vya mafunzo vilivyoidhinishwa vinaweza kupatikana kupitia tovuti ya NITA www.nita.go.ke

Tathmini na Udhibitisho

Vitengo vinavyotathminiwa ni:-

i. Utunzaji wa nyumbani
ii. Ustadi wa Maisha
iii. Mafunzo ya Kabla ya Kuondoka nchini
iv. Huduma ya kutunza Mtoto
v. Uuguzi wa Utunzaji wa Nyumbani

MAFUNZO KABLA YA KUONDOKA NCHINI

Maandalizi ya wakenya wanaoenda kufanya kazi ugenini kabla ya kuondoka ni muhimu katika kuwasaidia kujijulisha na mazingira mapya katika nchi ya kigeni.
Madhumuni wa mafunzo haya ni kuwatambulisha wahamiaji katika nyanja zote za ajira ya kigeni na hivyo kupunguza athari za "mshtuko wa kitamaduni" na wakati huo huo kutoa ufahamu kwa Wafanyikazi wahamiaji juu ya matarajio yao, fursa na changamoto katika ajira za kigeni.

Kuhitimu kwa mafunzo

Mafunzo ya kabla ya kuondoka nchini yako wazi kwa wakenya wote wanaotarajia kuhamia nchi za kigeni kwa ajili ya kufanya kazi.

Vitengo vya kozi

Mafunzo hayo ya kabla ya kuondoka nchini yanajumlisha vitengo hivi:

i. Maandalizi kabla ya kuondoka nchini,
ii. Mkataba wa huduma ya kigeni,
iii. Sheria na masharti ya ajira,
iv. Masuala ya kitamaduni na kidini katika nchi unakoenda,
v. Sarafu, viwango vya kubadilisha fedha,
vi. Njia za kutuma na kupokea fedha na fursa za uwekezaji,
vii. Haki na wajibu kazini,
viii. Ulinzi na usalama unapofanya kazi nje ya nchi
ix. Maeneo na jukumu la misheni za Kenya nje ya nchi.

Kwa Nini Mafunzo ya Kabla ya Kuondoka nchini ni Muhimu

i. Inakuza uhamiaji salama, halali na wa kibinadamu
ii. Husaidia kuzuia biashara haramu ya binadamu, ubaguzi, unyanyasaji wa Wafanyikazi katika hatua zote za mchakato wa uhamiaji.
iii. Inawahimiza Wafanyikazi kutoka Kenya kutunza ustawi wao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo
iv. Huwafahamisha Wafanyikazi kuhusu haki zao na njia za kulinda haki hizi
v. Hutayarisha wafanyikazi wahamiaji kuzoea mazingira mapya katika nchi wanakoenda
vi. Inatoa taarifa za kimsingi na chaguzi za kutuma pesa nyumbani na vile vile kusimamia bajeti na akiba zao
vii. Hutayarisha wafanyikazi wahamiaji kurejea nyumbani baada ya kumaliza muda wao wa umiliki katika nchi ya kigeni

AWAMU YA USAFIRI

Katika awamu hii mtu si mtafuta kazi tena lakini anachukuliwa kuwa mfanyikazi mhamiaji mtarajiwa. Awamu ya usafiri inajumlisha wakati ambapo mfanyikazi amepata hati zote zinazohitajika na idhini ya kusafiri na kuanza kazi katika nchi ya kigeni.

ORODHA YA MAMBO MUHIMU KABLA YA KUONDOKA NCHINI

i. Hakikisha kuwa kitengo cha kazi kilichotajwa kwenye visa yako inalingana na kazi ambayo umeajiriwa.
ii. Kumbuka kubeba hati zako halisi na nakala zake. Pia, acha nakala zaidi nyumbani kabla hujaondoka.
iii. Andika nambari zote za simu na maelezo mengine ya mawasiliano ya Misheni/Ubalozi wa Kenya katika nchi unayoenda.
iv. Hakikisha pasipoti yako ni halali kwa angalau miaka miwili.
v. Daima weka nakala za pasipoti yako na visa salama.
vi. Pata nakala ya mkataba wa ajira iliotiwa sahihi yako, mwajiri wako wa kigeni na Wakala wa Kuajiri.
vii. Unahitaji kufungua akaunti na benki yoyote nchini Kenya. Ikiwa unahitaji kutuma pesa kwa familia yako fungua akaunti ya pili ya pamoja ya akiba na mwanafamilia wako tofauti na akaunti yako kuu. Hii itakuwezesha kutuma mapato yako kwa usalama. Mwanafamilia wako anaweza kutoa pesa ukiwa nje ya nchi. Kumbuka nambari za SWIFT/NEFT/RTGS na IFSC za tawi na benki. Hizi ni nambari za kipekee zinazotambulisha na kuwezesha pesa kutumwa kwenye akaunti yako ya benki.
viii. Ni muhimu kupata sera ya bima ya usafiri kabla ya kuondoka Kenya, au bima nyingine yoyote kulingana na safari.
ix. Thibitisha ujue kiwango kinachoitajika cha mizigo cha shirika la ndege ili kuepuka gharama za ziada za mzigo wako.

TARATIBU ZA UWANJA WA NDEGE

Viwanja vya Ndege vyote vya Kimataifa vinahitaji wasafiri kuzingatia kwa ukamilifu sheria na itifaki wanapokuwa kwenye Uwanja wa Ndege ili kuhakikisha usalama katika uwanja huo. Kwa hivyo, ni muhimu kufahamu taratibu za uwanja wa ndege katika vitengo mbalimbali. Hapa kuna habari muhimu:

Safiri hadi Uwanja wa Ndege

i. Kuwa na ujuzi wa mfumo wa E-tiket
ii. Hakikisha jina la uwanja wa ndege, majina ya mashirika ya ndege, muda wa ndege ulioonyeshwa kwenye tikiti unaeleweka vyema
iii. Hakikisha usafiri umepangwa ili uweze kufika uwanja wa ndege saa 3 kabla ya muda wa safari ya ndege kama ilivyoonyeshwa kwenye tikiti ya safari.
iv. Weka tikiti yako, pasipoti, hati za visa, maelezo ya ndege, maelezo ya mfadhili au maelezo ya mtu ambaye atakupokea kwenye Uwanja wa Ndege na nambari za mawasiliano ya Ubalozi wa Kenya nchini unakoenda.

v. Hakikisha hautoi maelezo ya kibinafsi ya mawasiliano kwa watu wasiojulikana kwani unaweza kuwa katika hatari ya ulanguzi wa binadamu na kulaghaiwa.

Kwenye Uwanja wa Ndege

i. Hakikisha unaenda eneo sahihi la kuingia baada ya kuhakikisha kwenye mabango ya taarifa kwenye uwanja wa ndege. Wakati mwingine, maafisa wa forodha watafanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa hujabeba vitu vyovyote visivyoidhinishwa.
ii. Pasipoti yako na tikiti zinaweza kuangaliwa na afisa wa Uhamiaji kabla tu ya kuingia kwenye eneo la kuingia kwenye ndege. Mzigo wako pia utakaguliwa kwa usalama kwa mara ya pili
iii. Hakikisha hubebi vifurushi au mifuko yoyote ya watu wasiojulikana pamoja na mizigo yako kwani inaweza kuwa na vitu visivyojulikana au visivyo halali.

Katika ndege

i. Hakikisha umeketi kulingana na nambari ya kiti ulichopewa kwenye pasi ya kuabiri
ii. Hakikisha mzigo wako umewekwa kwenye cabin ya juu
iii. Sikiliza maagizo ya wahudumu wa ndege. Wapo kukusaidia. Waulize kama unahitaji taarifa/msaada wowote.
iv. Kumbuka utapewa viburudisho bila malipo ndani ya ndege
v. Hakikisha unatumia choo kama ulivyoagizwa na weka safi unapotoka.
vi. Kuwa na tabia ya utulivu na isiyosumbua wasafiri wengine.

Kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa kigeni

i. Hakikisha umejaza kwa usahihi kadi ya kuwasili. (Sehemu nyingi za mashariki ya kati hazitumii kadi ya kuwasili)
ii. Hakikisha kuwa muhuri wa Uhamiaji umewekwa kwenye pasipoti yako kama uthibitisho wa kuwasili
iii. Chukua mizigo sahihi kutoka kwa ukanda wa mizigo uliotengwa. Mzigo wako ukikosekana unaweza kutafuta usaidizi kwenye eneo la mizigo iliyopotea
iv. Hakikisha unafuata maagizo kwenye lango la kutokea kupitia forodha

Iwapo unasafiri kupitia uwanja wa ndege mwingine kabla ya Kufika:

i. Ni lazima ufahamu ikiwa ndege yako inasafiri moja kwa moja hadi nchi unakoenda au inapita kwenye uwanja mwingine wa ndege.
ii. Unaweza kuwasiliana na dawati la habari kwenye uwanja wa ndege ikiwa unahitaji usaidizi wowote
iii. Iwapo unahitaji kubadilisha safari yako ya ndege, fahamu kutoka kwa tikiti maelezo ya safari inayofuata ya ndege kama vile saa ya kuondoka na saa ya safari ya ndege na nambari za terminal.
iv. Mara tu unaposhuka kutoka kwa safari ya kwanza ya ndege, tafuta lango sahihi la kupanda ndege ya pili ndipo ufikie hapo bila kuchelewa.

v. Nenda kwenye lango la kutokea lililoonyeshwa baada ya kufuata taratibu muhimu za usalama
vi. Hakikisha mizigo wako utafika mwisho wakati mwingine unaweza kulazimika kubeba begi lako na kuliangalia tena
vii. Peana pasipoti yako, tikiti ya ndege na mizigo kwenye eneo ya Shirika la Ndege husika na upate pasi yako ya kupanda, kibandiko cha kukiri mizigo (Ikiwa unapitia sehemu ya kupita, hakikisha kuwa una pasi yako ya kuendelea ya kupanda)
viii. Tafadhali usiache mzigo wako wa mkono au mkoba wako bila kutunzwa ukiwa kwenye uwanja wa ndege.
ix. Hakikisha umejaza kadi ya kuanza kwa usahihi.
x. Nenda kwenye eneo la uhamiaji na uwasilishe pasi yako ya kusafiria, kadi ya kuanza safari na pasi ya kupanda ili uthibitishwe na uidhinishwe.
xi. Nenda kwenye lango la bweni kupitia maeneo ambayo hayalipiwi ushuru na lango sahihi la kupanda ndege kama inavyoonyeshwa kwenye pasi ya kupanda. Sikiliza matangazo ya umma na uingie na ukae kwenye eneo la kusubiri hadi tangazo la kupanda ndege litolewe na Wafanyikazi wa shirika la ndege.

BAADA YA KUPATA KIBALI CHA KUONDOKA KWENYE UWANJA WA NDEGE

Mara tu unapoondoka kwenye Uwanja wa Ndege katika eneo lako la Kazi, ni muhimu .

1. Tambua mwenyeji anayekupokea.

Kabla ya kuondoka kuelekea nchi ya kigeni, ni muhimu kubeba anwani za wakala au mwakilishi anayekupokea katika taifa hilo.

Thibitisha kitambulisho cha anayekulaki ili kuhakikisha kuwa unakutana na mtu sahihi (Kupitia kitambulisho au jina)

2.Wasiliana na jamii yako

Mara tu unapomtambua mtu anayekupokea, atakupeleka kwenye ofisi ya mawakala au kwenda kwa mwajiri wako. Unapaswa kuwasiliana na jamii pamoja na wakala wako wa nyumbani ili kuwajulisha kuwa umefika salama na mahali unapoishi.

3. Ijue ofisi ya wakala katika nchi ulikoenda

Tembelea ofisi ya wakala "maktab" katika nchi unakoenda kabla ya kuanza kazi hiyo. Hapa ndipo mahali ikiwa una tatizo na ajira yako unaweza kutafuta usaidizi kwanza.

4. Thibitisha mkataba

Wakala katika nchi ya kigeni anapaswa kukupa mkataba halisi kutoka kwa mwajiri ili ulinganishe na uliyo nayo. Wakati mwingine wanaweza kutofautiana. Zikitofautiana wasiliana na wakala wako wa nyumbani kwa usaidizi.

5. Ukiwa katika dhiki/Tatizo

Iwapo utakuwa katika dhiki wakati wowote unapofika wasiliana na wakala wa nyumbani, familia yako, wakala mwenyeji (Maktab) au Ubalozi wa Kenya nchini humo.

6. Jisajili katika Ubalozi wa Kenya

Unapotulia kwa mwajiri wako, pata muda wa kwenda kujiandikisha kwa ubalozi wa Kenya katika kipindi cha mwezi mmoja baada ya kuwasili.

KUFANYA KAZI NA KUISHI NJE YA NCHI

Huu ni wakati muhimu katika hatua za uhamiaji wa wafanyikazi na inategemea urefu wa mkataba. Ni wakati kuanzia kuwasili katika soko la ajira la kigeni hadi mwisho wa mkataba.

NINI WAFANYIKAZI WANAPASWA KUZINGATIA

Ili kuhakikisha ustawi na usalama wako kama mfanyikazi katika nchi ya kigeni, unapaswa kuwa mwangalifu kila wakati na kuripoti unyanyasaji wowote au tuhuma zinazotishia maisha yako. Yafuatayo ni baadhi ya masuala unayohitaji kuzingatia:-

1. Kunyang'anywa kitambulisho / hati za kusafiri

Kunyang'anywa au kuzuiliwa kwa hati za usafiri hasa au mali nyingine muhimu za kibinafsi ni mojawapo ya dhuluma zinazoripotiwa na Wafanyikazi wahamiaji. Unapaswa kuwa mumiliki wa hati zako kila wakati. Bila stagabathi muhimu, hauwezi kutembea kwa uhuru na kwa usalama au kuondoka katika nchi ya kigeni, na waweza kuwa hatarini ufungwe ikiwa utasimamishwa na kuhojiwa na polisi.

2. Kupunguza malipo, faini, au sheria haramu

Jihadhari ikiwa malipo yako ya kwenda nyumbani si yale uliyopewa na wakala wako.
Taratibu kadhaa kama zilizoorodheshwa zinachangia tofauti.

i) Mpangilio wa kuweka akiba za kulazimishwa - ambapo sehemu ya mshahara wako imezuiliwa na kuwekwa kwenye akaunti ya akiba ambayo huna umiliki hadi muda wako wa kazi ukamilike.

ii) Utozaji wa makato yasiyotarajiwa (na wakati mwingine kupita kiasi, yasiyoelezeka au kinyume cha sheria) kwa vitu kama vile chakula, nyumba au usafiri.

iii) Mishahara inazuiliwa, inacheleweshwa au haijalipwa; au ikiwa wafanyikazi wanalazimishwa kukubali malipo yasiyo ya pesa taslimu au malipo ya aina; na/au

iv) Katika baadhi ya matukio, Wafanyikazi wanatakiwa kutumia sehemu ya mshahara wao kuweka amana za fedha au ada za "usalama", k.m. kama "bima ya kukimbia".

3. Mwajiri kudhibiti akaunti za Benki

Tahadhari wakati mwajiri au wakala anasisitiza umiliki na udhibiti wa akaunti zako za benki.

4. Ukosefu wa uhuru wa kusitisha mkataba wa ajira

Waajiri na mawakala wanaweza kutumia njia mbalimbali za kulazimisha kuzuia uhuru wa Wafanyikazi kusitisha ajira, ikijumuisha:

i. Adhabu za uvunjaji wa mkataba ambazo zinawalazimisha wafanyikazi kusalia kazini kwa kuweka adhabu za kifedha kwa kukomesha mkataba kwa hiari au bila hiari;
ii. Vitisho visivyo rasmi vya upotevu wa mishahara, akiba au amana; na/au
iii. Tishio au matumizi ya vurugu, unyanyasaji au vitisho.

5. Kizuizi cha uhuru wa kutembea

Wafanyikazi wahamiaji wanaweza kuwekewa vikwazo vyovyote juu ya uwezo wao wa kuhamia kwa uhuru katika nchi ya kigeni, ikijumuisha:

i. Upangaji katika makazi yanayoendeshwa na mwajiri ni wa lazima kama sharti la kuajiriwa na/au kuendelea na ajira;
ii. Kuwepo kwa askari wa usalama au hatua nyingine za usalama mahali pa kazi au makazini kunazuia uhuru wa kutembea;
iii. Wafanyikazi wahamiaji hawako huru kurudi katika nchi yao ya asili wakati wa likizo ya malipo au likizo; na/au
iv. Kifungo au kufungiwa mahali pa kazi au majengo yanayohusiana nayo, k.m. makazi yanayoendeshwa na mwajiri.

6. Kutengwa

Jihadharini na kutengwa kwa kijiografia, kijamii, kitamaduni au hata lugha kunaweza kuwanasa wafanyikazi wahamiaji mahali pa kazi. Kwa kuwatenga wafanyikazi na kuwa tegemeo lao pekee cha chakula, habari na mawasiliano, madalali wa wafanyikazi wanaweza kuwafanya wafanyikazi wasiweze kuchukua hatua huru.

7. Vitisho na Vurugu

Vitisho na vurugu haipswi kuwaandama Wafanyikazi, lakini vinapotumiwa, vitisho na unyanyasaji ni njia bora za "kuwanyamazisha" Wafanyikazi, kuwafanya watii na kuogopa adhabu wanayoweza pata wenyewe au familia zao.

KUTUMA PESA KATIKA NCHI ASILI

Kuna majukwaa mbalimbali yanayorahisisha utumaji wa pesa kutoka nchi za kigeni.

1. Watoaji Huduma ya kutuma Pesa (Remittance Servirve Providers)

RSP ni huluki, inayofanya kazi kama biashara, ambayo hutoa huduma ya kutuma pesa kwa ada, moja kwa moja au kupitia mawakala. Hii inajumuisha (lakini sio tu) wanaofanya biashara ya kutuma pesa, wanaomiliki mitandao ya simu na benki. K.m. Safaricom, Western Union, MoneyGram, World Remit, Co-operative Bank, Equity Bank, Kenya Commercial Bank. n.k

2. Mashirika ya kutuma Pesa (Money Transfer Operator)

MTO hutoa huduma ya malipo asiyeweka amana ambapo huduma inahusisha malipo kwa kila uhamisho wa mtumaji hadi kwa mtoa huduma wa malipo. Hii inatofautiana na benki zinazochukua amana na kuruhusu uhamisho wa fedha kufanywa kutoka kwa amana hizo K.m. Western Union, MoneyGram, WorldRemit, Simba pay

3. Hawala

Hawala ni Kiarabu na maana ya ‘uhamisho’. Kwa ujumla inarejelea njia ya kutuma pesa nje ya mifumo ya kawaida ya benki. Njia hii ya kutuma pesa inategemea kufanya kazi kwa msingi wa uaminifu. Mfano wa shughuli ya hawala ni pale mfanyikazi katika nchi ya kigeni anataka kutuma pesa kwa wazazi nchini Kenya. Mfanyikazi huyo uhitaji huduma hawala nchini aliko, ambayo iko nje ya sekta rasmi ya kifedha.

KANUNI ZA KAZI

Kanuni za kazi ni adabu ambayo inasimamia matarajio ya tabia ya kijamii mahali pa kazi. Kanuni hii imewekwa ili "kuheshimu na kulinda saa, watu na taratibu." Hakuna makubaliano ya jumla kuhusu adabu ya kawaida ya kazi, ambayo inaweza kutofautiana kutoka kwa mazingira hadi mengine

Kama mfanyikazi mhamiaji, unatakiwa kuzingatia viwango vya juu katika utaratibu wako wa kila siku na kila mara ukubali na kuheshimu tofauti za kitamaduni ambazo zinaweza kuwepo. Daima jiendeshe kwa njia inayoamuru heshima.

FOMU YA NEA YA KUTOA TAARIFA ZA TAHADHARI

Jukwaa la kuripoti dhiki la NEA huruhusu Wafanyikazi katika mataifa ya kigeni na washikadau wengine kuripoti visa vya wafanyikazi kutoka Kenya walio na changamoto kupitia tovuti ya NEAIMS. Kisha NEA hutathmini na kuchukua hatua zinazohitajika au kupeleka malalamiko kwa mamlaka husika, ifaapo. Kuripoti kunaweza kufanywa kibinafsi au na mtu MWINGINE kwa niaba ya walio na changamoto au walioadhirika. Lazima wawe na Nambari halali ya Kitambulisho cha Kitaifa cha Kenya. Tembelea tuvuti www.neaims.go.ke ili kufikia fomu na kuripoti

JINSI YA KUPATA HABARI

i. **Tovuti ya wafanyikazi wahamiaji wa Kenya**

Hii ni tovuti maalum ya habari ya uhamiaji wa wafanyikazi www.kmw.go.ke ambayo inalenga kutoa taarifa muhimu na rasilimali kwa wanaotafuta kazi na wakenya wanaopanga kufanya kazi katika Ufalme wa Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Qatar. Tovuti inatoa taarifa

kuhusu masuala kuhusu: Jinsi ya kupata kazi katika ghuba, Nini cha kuangalia na kuepuka, Nini cha kufanya kabla ya kuondoka, Nini cha kufanya wakati wa kuwasili, Kufanya kazi na kuishi katika eneo la Ghuba; na jinsi ya kurudi nyumbani. Tovuti hii inaendelea kuimarishwa ili kufikia nchi zaidi.

ii. Vitabu vya kutoa muongozo kabla ya kuondoka nchini

Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA) chini ya msaada wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) ilitengeneza vitabu maalum vya habari ya nchi za Qatar, UAE, Saudi Arabia, Jordan, Oman, Poland na Uingereza ili kutoa mwongozo unaohitajika kwa Wafanyikazi wanaofanya kazi katika masoko hayo muhimu ya ajira. Vijitabu hivi vyote vinaweza kupatikana kwenye tovuti ya NEA www.nea.go.ke

iii. Ubalozi wa Kenya

Inashauriwa kujisajili na Ubalozi wa Kenya nchini unakoenda ili uweze kuhudumiwa kwa upesi unapohitaji habari na usaidizi katika hali ya dharura. Mawasiliano na maeneo ya balozi na balozi za Kenya zinaweza kupatikana kupitia vitabu maalum vya nchi kabla ya kuondoka kwenye tovuti ya NEA www.nea.go.ke. Zaidi ya hayo, Kenya imeanzisha ofisi za Labor Attaché nchini Qatar, Falme za Kiarabu (UAE) na Ufalme wa Saudi Arabia ili kusaidia katika utatuzi wa migogoro ya ajira na kazi na ukusanyaji wa data kuhusu Wafanyikazi wahamiaji wa Kenya.

KUREJEA NA KUUNGANIKA TENA NA JAMII

Hii ndio hatua ya mwisho ambapo mfanyikazi yuko tayari kurejea katika nchi ya asili baada ya kukamilisha wajibu wa ajira kulingana na mkataba au baada ya kusitishwa kwa mkataba na yeye mwenyewe au mwajiri.

ORODHA YA VITU VINAVYOHITAJIKA KABLA YA KUREJEA

Kabla ya kurejea nchini, unastahili kuhakikisha kwamba yafuatayo yamezingatiwa:-

1. **Cheti cha kutokuwa na pingamizi (No Objection Certificate)**

Pata kibali kutoka kwa mwajiri/ Cheti cha kutokuwa na pingamizi na cheti cha huduma

2. **Arifu familia yako na Ubalozi**

Mjulishe wakala, ubalozi wa Kenya na familia kuwajulisha kuwa namaliza au unaacha kazi na lini

3. **Hati za kusafiri**

Hakikisha hati za kusafiri ziko sawa. Hiyo ni passport yako ilio halali kisha upate tikiti ya ndege. Pia ijulishe shirika la ndege kuhusu mzigo wako ili kujua gharama na kile kinachoruhusiwa.

4. **Vifungu vya kusitisha mkataba**

Ni muhimu kuangalia mkataba wako kwa vifungu vya kusitisha. k.m. kipindi cha kupeana notisi n.k.

5. **Malipo ya mwisho**

Shughulikia ada zako za mwisho na ulipwe. Tafadhali kumbuka kuwa pesa taslimu zaidi ya USD 5,000 zinahitaji kutangazwa kwenye eneo ya uhamiaji na kodi katika uwanja wa ndege.

6. **Tuma notisi au badala ya kulipa**

Unahitaji kutoa muda wa notisi kulingana na mkataba wako. Ikiwa sivyo, unahitaji kulipa badala ya muda wa notisi

MAANDALIZI KABLA YA KURUDI NYUMBANI

i. Kamilisha ahadi zako za kazi na umjulishe mwajiri wako kabla ya kuondoka ncini ya kigeni.
ii. Yapaswa uondoke katika nchi unayofanyia kazi kabla ya muda wa visa kuisha; ikiwa umetuma ombi la kuongeza muda wa visa yako na ikakataliwa, unapaswa kuondoka nchini humo.
iii. Baada ya muda wa mkataba wa ajira kukamilika, mwajiri wako anatakiwa kupanga safari yako ya kurudi Kenya na kulipia tikiti ya ndege kulingana na Sheria ya Uhamiaji.
iv. Katika hali ya dharura, kumbuka kwamba hati ya kiapo ambayo Wakala wa Uajiri huwasilisha kwa NEA. Inasema kwamba wakala lazima awajibikie mfanyikazi, kwa hivyo wakala atalazimika kufanya kazi na mwajiri wako ili kukurudisha Kenya.
v. Unahitaji kupata cheti cha kukosa pingamizi (No Objection Certificate) kutoka kwa mfadhili/mwajiri wako kabla ya kuondoka katika nchi ya ajira.
vi. Mwajiri wako atalazimika kukulipa mshahara wako wa mwisho pamoja na malipo mengine yoyote ambayo hayajalipwa.
vii. Unapaswa kutoa pesa zozote zilizobaki kwenye akaunti yako ya benki katika nchi unayofanyia kazi (ikiwa ulifungua akaunti katika benki huko).
viii. Tuma pesa hizo kwa akaunti ya NRE katika benki ya Kenya au uzitume nyumbani kupitia mbinu nyingine zozote ambazo zilielezwa kuhusu utumaji pesa.
ix. Hakikisha una hati zako asili (pasipoti, visa n.k.). Ikiwa mwajiri wako ana hati zako halisi na hataki kuzirejesha, wasiliana na Misheni/Chapisho la Kenya mara moja na uandikishe malalamiko.
x. Ikiwezekana, hakikisha kwamba unapata barua za uidhinishaji ambazo zinaorodhesha ujuzi uliojifunza na uzoefu wa kazi uliopata wakati wa ajira yako.

SAFARI YA KUREJEA NCHI ASILIA

i. Kumbuka kutumia uwanja wa ndege na taratibu zilezile za ndege ulizotumia ulipowasili.

ii. Hakikisha una hati zako zote halisi (pasipoti, NOC, visa n.k.) pamoja nakala sawa.

iii. Iwapo umebeba fedha za kigeni zenye thamani ya USD 5,000 au zaidi, unatakiwa kuzitangaza kwenye uwanja wa ndege nchini Kenya na utie sahihi kwenye fomu ya kuthibitisha hilo.

iv. Unaweza kubeba vitu vya kibinafsi na vya nyumbani vilivyotumika kama vile vyombo vya jikoni na vifaa vidogo vya kielektroniki (kwa vifaa vikubwa kama vile TV na friji kubwa zaidi ya lita 300, utahitaji kulipa ushuru wa kuagiza ikiwa unawarejesha Kenya).

KUUNGANA NA JAMII BAADA YA KUREJEA

i. Wahamiaji wanaorejea nyumbani mara nyingi hupata ugumu wa kujumuika katika jamii zao. Huenda wasitumie vyema ujuzi wao au akiba zao.

ii. Baada ya kuzoea mishahara ya juu katika nchi za kigeni, wafanyikazi wanaweza kutatizika kupata kazi za nyumbani ambazo wanaweza kukubali.

iii. Walioathiriwa zaidi ni waathiriwa wa ulanguzi ambao watarejea bila fedha na huenda wasikubalike kwa urahisi katika jamii zao za nyumbani.

iv. Wahamiaji wanaweza kutatizika kutosheka na familia na jamii wanaporejea ikiwa wameishi nje kwa muda mrefu na wamezoea tamaduni na mitindo ya maisha katika nchi za kigeni.

v. Huenda umehifadhi kiasi kikubwa cha pesa wakati unafanya kazi nje ya nchi lakini unahitaji kuzitumia vizuri mara tu unapofika nyumbani. Ukosefu wa ujuzi wa jinsi ya kutumia akiba ya mtu vizuri ni changamoto kubwa kwa wahamiaji wengi wanaorejea.

vi. Serikali imezindua idadi ya mipango ya kuwajumuisha wahamiaji ili kuwasaidia kuekeza vyema wanaporejea njini.

vii. Wahamiaji, hata kama wamekuza ujuzi wakati wa kufanya kazi nje ya nchi, wanaweza kutokuwa na ujuzi wowote ulioidhinishwa, ambao unaweza kufanya vigumu kuhamia nchi nyingine baada ya kurejea nyumbani, kulingana na utafiti wa ILO.

JINSI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

i. Ni sharti ukubali kuwa uhusiano wako na familia yako, hasa mume/mke na watoto wako, utakuwa umebadilika ikiwa umekuwa mbali nao kwa muda mrefu. Ni muhimu kutumia muda kuzungumza nao ili kujenga upya mahusiano huyo.
ii. Wasiliana na marafiki, jamaa na watu katika jamii yako ambao wamehamia nje ya nchi kwa ajili ya kazi hapo awali; wanaweza kukupa ushauri na usaidizi wa kufaa.
iii. Fikia mtandao wako mpana wa marafiki na familia kwa fursa zinazohusiana na ajira, usaidizi wa kuanzisha biashara na kuwekeza akiba yako kwa busara.

MASWALI YA MARA KWA MARA KUHUSU UHAMIAJI WA WAFANYIKAZI

1. Ni nani anayestahili kufanya kazi nje ya nchi?

Raia wa Kenya yeyote mwanamume au mwanamke aliye na umri wa miaka 18 na kuendelea, mwenye akili timamu na mwenye rekodi ya mwenendo mzuri.

2. Je! Naweza pata vipi habari kuhusu kazi nje ya Kenya?

Waweza pata habari hizi;

i. Kupitia mashirika ya ajira yaliyosajiliwa,
ii. Kupitia tovuti k.m. www.neaims.go.ke,
iii. Kupitia vyombo vya habari na
iv. Juhudi za mtu binafsi au/ rufaa

3. Je, ninawezaje kujua kama ofa ya kazi ni ya kweli au ya uwongo?

Ikiwa ni wakala wa ajira, bainisha kama wakala:

Anayekushughulika ameidhinishwa au amepewa leseni na Mkurugenzi wa Ajira, Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira na ana utaratibu unaofaa wa kazi na mtu anayefanya biashara naye ameunganishwa kihalali na wakala huyo.

Thibitisha kama wakala,

i. Ana ofisi,
ii. Imesajiliwa kama Kampuni ya Dhima ndogo na msajili wa Makampuni,
iii. Imepewa leseni na Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA), na
iv. Hutoza ada au kamisheni yoyote.

Vilevile, sisitiza juu ya:

i. Matoleo halisi ya kazi kutoka kwa mwajiri,
ii. Sheria na masharti ya kazi, na
iii. Stakabadhi rasmi iwapo malipo yoyote yamefanywa

Unapaswa:

i. kutuma ombi katika ofisi iliyosajiliwa ya wakala wa uajiri pekee. Ikiwa uajiri unafanywa nje ya anwani ya ofisi iliyosajiliwa, thibitisha ikiwa ina mamlaka iliyotolewa na Mkurugenzi wa Ajira au umeruhusiwa kuendesha shughuli za kuajiri nje ya ofisi zao.

ii. Uliza nakala ya mkataba wa ajira na usome sheria na masharti.

iii. Usilipe ada yoyote isipokuwa kama umeajiriwa na kutia Sahihi mkataba wa ajira.

iv. Hakikisha unapewa risiti mara unapolipa malipo yoyote

TANBIHI

Orodha ya Mashirika ya Kibinafsi ya Kuajiri Walio na leseni nchini Kenya imechapishwa kwenye tuvuti www.neaims.go.ke

Ikiwa unatafuta kazi kibinafsi bainisha kama:

Kazi ni za kweli kutoka mwanzo. Wakati fulani ni vigumu kubaini uhalisia wa kazi zinazotangazwa kupitia tovuti.

Kwa hivyo, inashauriwa:

i. Kutafuta taarifa zaidi hasa pale ambapo waombaji wanatakiwa kulipa kiasi kikubwa cha pesa kabla ya kushughulikia maombi.

ii. Kuwasiliana na ubalozi wa nchi unakoenda ili kujua kama kampuni ya uajiri inajulikana na sifa zake.

iii. Kuhakikisha iwapo mwajiri wako wa baadaye atashughulikia mahitaji yako (tikiti ya ndege, visa ya kazi, n.k.),

Lazima uhakikishe kuwa:

i. Una haki kushughulikiwa na mashirika husika ya serikali kama inavyohitajika

ii. Visa au kibali chako cha kazi na mkataba wa ajira uidhinishwe na ubalozi wa Kenya au ubalozi mdogo wa Kenya katika nchi unakoenda.

iii. Unafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na zahanati au hospitali inayotambulika

iv. Unapata mafunzo elekezi ya kabla ya kuondoka na taasisi ya mafunzo iliyoidhinishwa na NITA.

4. Je, sheria inapunguza ada ambazo wakala wa ajira anaweza kutoza?

Ndiyo

Mashirika ya ajira hunitoza ada kwa huduma zinazotolewa. Ada hiyo lazima hata hivyo iidhinishwe na mkurugenzi wa uajiri na lazima iwe ndani ya masharti ya kisheria.

Katika kesi hiyo, waombaji lazima wapewe risiti rasmi kwa kiasi kilicholipwa.

Risiti lazima iSahihiwe na mtu aliyepokea malipo, na lazima ionyeshe:-

i. jina la mwombaji,
ii. jina na anwani ya wakala wa ajira,
iii. tarehe na kiasi cha ada
iv. madhumuni ya ada au amana.

Hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha usalama wako:

Kabla ya kuondoka nchini:

i. Hakikisha kwamba ofa ya kazi ni ya kweli.
ii. Hakikisha kwamba unasafiri na nyaraka sahihi na za kisheria. Nchi nyingi zinahitaji utume maombi ya visa ya kazi ikiwa unapanga kufanya kazi katika nchi hiyo.
iii. Hakikisha kwamba Mkataba wa Utumishi wa Kigeni (mkataba wa ajira) umethibitishwa na Afisa wa Kazi
iv. Tafuta tafsiri kutoka kwa shirika linalotambulika iwapo hati yoyote iko katika lugha ya kigeni
v. Kuwa na mawasiliano ya watu na mashirika ambayo yanaweza kutoa usaidizi mara tu unapowasili.
vi. Hakikisha una maelezo ya mawasiliano ya Ubalozi wa nchi yako au Tume ya Juu katika nchi ambayo ungependa kupata kazi.
vii. Pata maelezo ya Ubalozi wa Kenya, Balozi wa ubalozi katika nchi unakoenda
viii. Mjulishe Ubalozi, Tume Kuu au ubalozi unapowasili kwamba uko nchini na uwape anwani na maelezo ya mawasiliano.

ix. Pata maelezo ya simu za usaidizi

x. Hakikisha umepata kibali

xi. Hakikisha umepitia semina elekezi kabla ya kuondoka

xii. Hakikisha kwamba unawajulisha wanafamilia wa karibu

xiii. Toa maelezo ya jamaa yako wa karibu

4. Je, shirika la ajira linatakiwa kutoa nakala za mikataba?

Ndiyo. Mashirika ya ajira lazima yawape waombaji nakala ya mkataba wowote ulioingiwa kati ya wakala wa ajira na mwombaji.

5. Ni nyaraka gani ninahitaji kabla ya kusafiri na nitazipata kutoka wapi?

Hati zinazohitajika kabla ya kusafiri zimeorodheshwa katika jedwali 1 hapa chini, ikijumuisha wapi na jinsi ya kuzipata

Jedwali la 1*:* Vyeti vinavyohitajika Mahitaji kabla ya usafiri na mahali pa kupata

Ninahitaji nini?	**Je, nitaipata wapi?**	**Je, ninaipataje?**
Pasipoti Halali ya Kenya	Mkurugenzi wa Huduma za Uhamiaji • Nairobi – Nyayo House • Mombasa • Kisumu – Re-insurance Plaza	Unahitaji:- - Cheti halisi cha Kuzaliwa - Kitambulisho cha Taifa - Pasipoti mbili za rangi (Sio picha yangu) - Fomu ya maombi iliyojazwa - Cheti cha Kibali cha Polisi - Ada ya kufanya upya pasipoti - Msajiliwa kutembelea -
Cheti Halisi cha Kuzaliwa	Idara ya Usajili wa Raia - Msajili wa watuwanaozaliwa na kufa	Unahitaji:- Ripoti ya mahali ulipozalwa na kuandikishwa:- - kukiri kwa Taarifa ya Kuzaliwa (ABN)

		- Ada ya cheti - Rekodi ya marekebisho ya ada ikiwa marekebisho yoyote yanahitajika. Iwapo haukusajiliwa wakati ulipozaliwa:- - Kujaza fomu za usajili wa kuzaliwa - Kadi asili ya Kitambulisho - Cheti cha kuhitimu shule - Kadi ya ubatizo - Kwa watoto, kitambulisho/Kadi za wazazi - Kadi ya kliniki, iwapo itapatikana - Wale walio katika ajira ya kudumu na ya pensheni, barua kutoka kwa mwajiri inayoonyesha tarehe ya kuzaliwa katika faili ya kibinafsi. - Ada ya cheti ni kama ifuatavyo: - Aliyezaliwa kabla ya wilaya kutangazwa kuwa usajili wa lazima - Kshs.50/= - Aliyezaliwa baada ya wilaya alitangazwa kuwa usajili ni wa lazima - kshs.150/=
Cheti cha kibali cha polisi	Makao Makuu ya CID ya Nairobi kwenye Barabara ya Kiambu	Unahitaji:- - Kujipeleka kibinafsi - Nakala ya Kadi ya Utambulisho - Uwe na Shilingi 1,000/=
Mkataba halali wa huduma	Wakala wa Ajira	Unahitaji:- - nakala ya Fomu za Huduma za Mkataba wa Kigeni (LD21) kutoka Wizara ya Kazi. -
Cheti cha Matibabu	- Taasisi ya matibabu inayotambuliwa - Taasisi ya matibabu iliyopendekezwa na mwajiri mtarajiwa au wakala. -	Unahitaji:- - Nakala ya fomu za Mkataba wa Kigeni wa Huduma (LD 21) kutoka Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kazi na Ulinzi wa Jamii. - Ada ya uchunguzi wa matibabu (kulingana na taasisi)
Kibali cha Kazi	Nchi lengwa	Unahitaji kutuma maombi kupitia ubalozi au mawakala husika.
Visa ya kusafiri	Balozi za inchi zilizolengwa	Unahitaji:- - Kutuma Ombi - Pasipoti

HITIMISHO

Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira bado imejitolea kuwapa wafanyakazi ujuzi unaohitajika katika soko la ajira na pia kutoa taarifa zitakazolinda maslahi na usalama wao. Kufikia lengo hili, Mamlaka iliimarisha uratibu wa mafunzo ya kabla ya kuondoka nchini na ratba elekezi kwa wahamiaji wanaotoka nje ya nchi ili kuwafahamisha maarifa na ujuzi unaohitajika ili kukabiliana na mazingira ya kazi katika nchi za marudio ya kazi. Watafuta kazi wanahimizwa kila mara kushirikiana na Mashirika ya Kibinafsi ya Kuajiri (PRAs) na kutumia njia zinazokubalika kisheria kupata ajira za kigeni.

Mamlaka ya Kitaifa ya Ajira (NEA)
Seasons, Kasarani
S.L.P 25780-00100
Nairobi-Kenya
www.nea.go.ke